**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba za Simu**
**Mkuu wa Shule: 0714155827 /0782990889**
**Makamu Mkuu wa Shule: 0683081454**
**Matron/Patron: 0783141575**

**Shule ya Sekondari Nkowe**
**S.L.P 76,**
**Tarehe ……….………**

.

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi..........................................................**
**S.L.P...................................................................................................**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NKOWE HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA MKOA WA LINDI MWAKA ………………….**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka …………….. na atasoma tahasusi ya ….….……

Shule hii ni ya bweni na ipo Kijiji cha **Mpumbe**, wilaya ya Ruangwa mkoa wa Lindi. Usafiri kwa watakaotoka njia ya **Dar es Salaam** kuna mabasi yanatoka **Dar es Salaam** hadi **Ruangwa** moja kwa moja kutokea kituo cha mabasi cha Temeke mwisho au Mbagala Rangi 3 watashuka kijiji cha Mpumbe, ndipo shule ilipo. Kwa watakaotokea njia ya **Songea** kuna magari yanatoka **Songea - Lindi - Mtwara** watashuka kijiji kinaitwa Nanganga kisha watapanda daladala zinazoelekea **Ruangwa** na watashuka kijiji kinachoitwa **Mpumbe**. Kutoka Mpumbe kijijini hadi shuleni kuna umbali wa takribani mita 750. Ambapo kwa usafiri wa pikipiki ni **shilingi elfu moja** kutoka barabarani hadi shuleni.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **……………….** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **……………..** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **…………………..**

## 1. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 1.1 Sare za Shule

**Sare za Shule kwa Wavulana.**

(i) Suruali mbili (2) ndefu rangi ya kijivu (gray colour) mbele iwe na rinda na chini iwe na upana wa wastani. (Zinapatikana shuleni).

(ii) Shati mbili (2) nyeupe zenye mikono mirefu na yenye kola shingoni.

(iii) Viatu vya ngozi jozi mbili (2) viatu visiwe na urembo wowote na wala visiwe vya kupanda na viwe vya kufunga na Kamba.

(iv) Soksi imara nyeusi jozi mbili (2)

(v) Nguo za michezo, bukta moja (1) na jezi yake rangi ya zambarau, Tracksuit moja (1) nyekundu na viatu vya michezo.

(vi) Aje na sweta moja (1) rangi ya kijivu (gray colour) liwe la kufuma.V-shape.

(vii) Suruali mbili (2) rangi ya damu ya mzee (maroon) shamba dress zenye urefu na upana wa heshima na zilizoshonwa kwa unadhifu na sio kwa mapambo.

**Sare za Shule kwa Wasichana.**

(i) Sketi ndefu mbili (2) rangi ya kijivu (gray colour) zenye V mbele isiyobana na isiwe na mpasuo. (Zinapatikana shuleni);

(ii) Shati mbili (2) nyeupe zenye mikono mirefu na yenye kola shingoni au nusu kanzu kwa wale tu wanaovaa hijabu (ashone hijabu nyeupe na ya bluu ifunike kifua na pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama);

(iii) Viatu vya ngozi jozi (2) viatu visiwe na urembo wowote na wala visiwe vya kupanda na viwe vya kufunga na Kamba.

(iv) Soksi imara nyeusi jozi mbili (2)

(v) Nguo za michezo, bukta moja (1) na jezi yake rangi ya zambarau, Track suit moja (1) nyekundu na viatu vya michezo.

(vi) Aje na sweta moja (1) rangi ya kijivu (gray colour) liwe la kufuma.V-shape;

(vii) Gauni mbili (2) rangi ya damu ya mzee (maroon colour) shamba dress zenye urefu na upana wa heshima na zilizoshonwa kwa unadhifu na sio kwa mapambo na juba la rangi ya maroon.

(viii) Baibui nyeusi kwa waislamu ya kuendea msikitini na juba jeusi

## 1.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari ya kutosha yasipungue 14 Quire 3
ii. **Ream (A4)** bunda Nne (4).
iii. Graph pads 1, kalamu za kutosha (pen and pencils)
iv. Faili Folder la kaki 1 na la plastic 1.
v. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika;
vi. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
vii. Scientific Calculator;
viii. Godoro la sponji moja2½,x6''
ix. Mashuka Jozi 2 za rangi ya bluu bahari iliyoiva, blanket 1, mto na foronya yake 1, chandarua 1 chenye dawa rangi ya bluu
x. Nguo za ndani za kutosha, taulo moja
xi. Sanduku imara la chuma(trunker) na kufuli.
xii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
xiii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xiv. Jembe 1, squizer/mopper 1 na fyekeo 1 (kwa tahasusi ya CBG na PCB), reki 1,brashi ya chooni 1 na panga 1 ( kwa tahasusi ya PCM),
xv. Mifagio 2 ( laini1 na mgumu 1 ya dukani),
xvi. Dawa ya ya chooni Lita tano (5).

**Tanbihi**: Vifaa vifuatavyo vinapatikana kwenye duka shuleni lakini ni hiari ya mwanafunzi kununua kwa bei zifuatazo:

- Godoro = Tsh 45,000/=.
- Fyekeo= Tsh 6,000/=
- Jembe= Tsh ,7000/=
- Reki= Tsh 8,000/=
- Panga= Tsh 6,000/=
- Fagio laini = Tsh 5,000=
- Fagio ngumu= TSH 4,000/=
- Dawa ya chooni lita 5= Tsh12,000/=
- Ndoo ndogo lita 10= Tsh 3,500/=
- Brash ya chooni= Tsh 3,500/=
- Mopper= Tsh 7,500/=
- Squizer= Tsh 7,500/=

- Scientific Calculator = 45,000

**NB: Mwanafunzi aje na kitambulisho cha bima ya afya au fedha Tsh 54,000/= kwa ajili ya kukata bima ya afya**

### 1.3 Michango mbalimbali- Shule za Bweni

**Michango ya shule ilipwe kwenye Akaunti ya Shule Na. 71101100098 NMB (Nkowe Secondary School Recurrent Account**) na kisha kuwasilisha **bank pay slip** siku utakayoripoti shuleni na iandikwe majina kamili ya mwanafunzi.

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

### 2.1. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu– TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 2.2. Sheria na Kanuni za Shule

(i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
(iii) Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
(iv) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na;

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**2.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na wanajamii;

v. Kupigana mwanafunzi mwenzio, kumpiga mwalimu au mtu mwingine;

vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote

vii. Kufuga ndevu;

viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

ix. Uvutaji wa sigara;

x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;

xii. Kusababisha mimba;

xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yanayovunja sheria za nchi;

xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;

xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;

xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3 Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi / Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**4** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**Karibu sana.**

**Saini ya Mkuu wa Shule**

*VLM*

**Jina la Mkuu wa Shule** **VICTORY LEONARD MBILA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

THE HEADMASTER
NKOWE HIGH SCHOOL
P.O. Box 76
RUANGWA

**TAHADHARI**

Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa**.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU** MWANAFUNZI**/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

➢ **MAWASILIANO**

- **MKUU WA SHULE: 0714155827** /0782990889
- **MAKAMU MKUU WA SHULE: 0683081454 /0663670483**
- **MWANDAMIZI TAALUMA: 0789369014**
- **MWANDAMIZI MALEZI: 0783141575**

**TAARIFA BINAFSI KUHUSU MWANAFUNZI**

**(Form hii ijazwe na irudishwe shuleni)**

1. Jina la Mwanafunzi…………………………………...………kidato……………………
2. Kabila la Mwanafunzi……………………………………………………………….
3. Tarehe ya Kuzaliwa………./………/……………… .
4. Wilaya alikozaliwa mwanafunzi……………………… Mkoa………………………………….
5. Dini ya mwanafunzi ………………………………..
6. Tatizo la Kiafya la mwanafunzi ……………………………………………
7. Jina kamili la baba ……………………………………..…
8. Anuani kamili ……………………………..…..... .simu………………..,………
9. Kazi ……………………………………………………….
10. Jina kamili la mama……………………………………………………
11. Anuani kamili……………..…………………………..………… simu…………………..
12. Kazi…………………………………….
13. Jina kamili la mlezi anayemhudumia mwanafunzi ............................................................
14. Uhusiano wa mwanafunzi na mlezi…………………………………………………………
15. Anuani kamili…………………...…….simu………….. ……kazi yake……………..
16. Baba na mama **wanaishi pamoja / wametengana** (kata isiyohusika)
17. Uwepo wa wazazi: Baba YUPO/HAYUPO kama amefariki, lini …………………………….

18. Mama YUPO/HAYUPO kama amefariki lini……………………………..

19. Orodha ya ndugu wengine ambao shule inaweza kuwasiliana nao moja kwa moja

| NA | JINA | UMRI | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

**PRESIDENT'S OFFICE,**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

Nkowe secondary school
P.O.BOX 76
**Ruangwa-Lindi**

REF: NO.................................................
**To The Medical Officers (District/regional)**
.................................................................
Sir/Madam,

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION TO**
***(Name of student)........................................................................***

Please examine the above named student and give the report regarding his/her suitability for undertaking secondary school studies.

1. Eye sight.......................................................................................................
2. Hearing.........................................................................................................
3. Speech..........................................................................................................
4. Venereal diseases.........................................................................................
5. Neurosis.........................................................................................................
6. Pregnancy (for girls only)...............................................................................
7. T.B test...........................................................................................................
8. Syphilis test....................................................................................................
9. Urine test........................................................................................................
10. Ears test........................................................................................................
11. Spleen...........................................................................................................
12. Abdomen.......................................................................................................

**ANY ADDITIONAL INFORMATION:**
(Physical defeats or impairment, infection, family diseases Etc)
..................................................................................................................................
……………………………………………………………………………………………

**COMMENTS**
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................

I certify that the above student is suitable/unsuitable for secondary school studies. If unsuitable give reasons
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................

**Name of Medical Officer.....................................................Signature.......................................**
**Date........................................................................... Official stamp...................................**

## AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi… ........................................................................................... ambaye ni mzazi wa………………………………………….. Aliyetoka shule ……………….…………………

wilayani……………………………………………….mkoa…………………….………………

Nimesoma na nimeyaelewa maagizo ya kujiunga na shule hii na nina ahidi kuwa nitajitahidi kumpa mahitaji mengine mwanangu aliyetajwa hapo juu hadi atakapomaliza ELIMU YA SEKONDARI.

Sahihi………………………………………………Tarehe………………………………….

## AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi…............................................................................... wa kidato cha……………….
Nimesoma na kuzielewa sheria za shule na naahidi kuzitii na kuzitimiza taratibu zote zilizowekwa.

Sahihi………………………………………………Tarehe………………………………….